

# **CHAKULA CHA BWANA**

Chakula cha Bwana ni nini? Kwa nini kushiriki? Tushiriki mara ngapi? Haya ni maswali katika akili za wengi. Chakula cha Bwana kilianzishwa na Bwana mwenyewe kama kumbukumbu kwa ajili ya mateso yake kutokana na dhambi zetu (Mt. 26:26-29). Leo Wakristo wanaadhimisha jambo hili kukumbuka tukio kuu la vizazi vingi, kifo cha Kristo. Kushiriki katika hali ya kumpendeza Mungu, chakula hiki ni vema kiwe na vitu halali.

## **Vitu Halali**

Mkate na uzao wa mzabibu ndivyo vitu vya msingi. Ingawa si mwili na damu halisi, mkate ni ushirika wa mwili wa Kristo na kikombe ushirika wa damu yake (Lk. 22:12-20). Wakristo wanapoizingira meza hii mioyo yao inachochewa kwa uaminifu kutambua maisha yake yenye utukufu yalivyotolewa kafara na kifo chake msalabani kwa ajili ya ulimwengu mwovu.

## **Washiriki Halali**

Yesu alisema angekunyuwa kwa kikombe hiki pamoja na wale waliomo katika Ufalme wa Baba (Mt. 26:29) waamini waliobatizwa waliendelea kwa juhudhi katika kumega mkate, (Mdo. 2:42). Wanafunzi walikuja pamoja kukutanika Siku ya Kwanza ya juma kumega mkate (Mdo. 20:7). Wale waliomo katika Kanisa la Bwana ndio watu halali wa kushiriki Chakula cha Bwana. Lakini hakuna aliye na haki ya kukataza au kufunga ushirika huo kwa sababu Paulo alisema “Lakini mtu ajihoji mwenyewe, na hivyo aule mkate, na kukinywea kikombe,” (1 Kor. 11:28).

## **Roho Inayostahili**

Isipokuwa katika jicho lenye akili, “Kuupambanua mwili, anakula na kunywa hukumu ya nafsi yake,” (1 Kor. 11:29). Kwa sababu baadhi ya Wakorintho walishiriki Chakula cha Bwana katika hali isiyostahili na wala taadhima katika Roho, wakawa dhaifu na wasiojiweza (1 Kor. 11:30). Katika kushiriki, afanye hivyo kwa kumbukumbu..... “Fanyeni hivi...kwa ukumbusho wangu” na kwa kujihoji, “lakini mtu ajihoji mwenyewe” na kwa matazamio, “mwitangaze mauti ya Bwana hata ajapo,” (1 Kor. 11:25, 26, 28).

## **Muda Ustahilio**

Katika Agano Jipyawakristo wanashiriki Chakula cha Bwana Siku ya Kwanza ya Juma (Mdo. 20:7). Mara ngapi? Kila ijapo Siku ya Kwanza ya Juma. Kama vile Wayahudi walivyojua amri ya kuadhimisha kila Siku ya Kwanza ya Juma. Kwa kuwa hakuna kabisa mamlaka yanayotuhitaji katika Agano Jipyawakristo kuadhimisha kwa mwaka, nusu mwaka, robo au kila mwezi, ni lazima tufuate Kanisa la Kwanza na kushiriki kila juma. Hivyo, dhahiri, ni salama na hatuwezi kutiliwa mashaka.

Agano Jipya huwaamuru Wakristo kufanya matoleo ya vitu vyao vya kimwili kwa Bwana kila siku ya kwanza ya juma na kwa vitendo kila kundi la dini lafanya hilo (I Kor. 16:1-2). Na bado mamlaka hiyo hiyo isemayo tutoe kila Siku ya Kwanza ya juma husema tushiriki Meza ya Bwana kila Siku ya Kwanza ya juma.

Hii yaelezea namna ambavyo Kanisa la Yerusalemu lilivyodumu “Katika kumega mkate” na jinsi Paulo ambavyo angeweza kusema Wakorintho wakawa wakidumu katika ushirika (Mdo. 2:42; 1 Kor. 11:25).

Ni kweli ni jambo la hatari Mkristo yejote anaporuhusu kipindi au saa hiyo nzuri iondolewe moyoni mwake kwa visingizio vidogo vidogo tu. Chakula hiki cha Bwana kimetolewa kwa ajili ya afya ya Kiroho na ustawi wa watoto wa Mungu na anafanya makosa ye yote anayeacha kushiriki Meza ya Bwana katika siku yo yote ya kwanza ya juma.

[www.kanisalakristo.com](http://www.kanisalakristo.com)